THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/2 **KISWAHILI 2**

(Kwa Watahiniwa Wasiokuwa Shuleni tu)

*Muda: Saa 3* *Ijumaa, 12 Februari 2010 asubuhi*

---

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina maswali **kumi na nne (14)** katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano (5)** kwa kuchagua swali **moja (1)** kutoka **kila sehemu**.
3. Kila swali lina alama **ishirini (20)**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 6 zenye maandishi

TATA PRINT-2010

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 20)

## FASIHI KWA JUMLA

1. "Mikakati ya ukombozi wa Tanganyika na Zanzibar ilihamasishwa na kazi za fasihi." Jadili hoja hiyo ukitumia mifano mahsusi.

2. "Upekee wa lugha ya fasihi na jinsi inavyotumika katika fasihi, inabainisha kazi ya fasihi na kazi nyinginezo zisizo katika taasisi hiyo. "Fafanua kauli hiyo kwa kutoa hoja nne (4).

3. "Mhakiki ni daraja kati ya msanii na jamii anayoiandikia." Jadili hoja hiyo kwa kutumia kazi mbili (2) za fasihi andishi ya Kitanzania.

## SEHEMU B (alama 20)

## USHAIRI

| | | |
|---|---|---|
| Kimbunga | - | **H. Gora** |
| Mapenzi Bora | - | **S. Robert** |
| Chungu Tamu | - | **T.A. Mvungi** |
| Fungate ya Uhuru | - | **M.S. Khatib** |

4. "Mfumo wa jamii hutawala akili ya mshairi na kazi yake." Jadili kauli hiyo kwa kutumia hoja nne (4) kutoka kila kitabu katika diwani mbili (2) ulizosoma.

5. "Ushairi ni kichocheo cha mabadiliko katika jamii." Eleza mchango wa washairi katika kuleta mabadiliko, kwa kutumia hoja nne (4) kwa kila kitabu, kutoka katika diwani mbili (2) ulizosoma.

6. "Kila taasisi katika maisha ya binadamu inaguswa na ushairi". Thibitisha hoja hiyo kwa kutumia diwani mbili (2) ulizosoma.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C ( alama 20)

### RIWAYA

| | | |
|---|---|---|
| Usiku Utakapokwisha | - | Mbunda Msokile |
| Kufikirika | - | S. Robert |
| Mfadhili | - | Hussein Tuwa |
| Vuta N'kuvute | - | Shafi Adam Shafi. |

7. "Uhai wa riwaya utatokana na dhamira zilizojadiliwa na msanii." Thibitisha kauli hiyo ukitumia hoja nne (4) kwa kila kitabu kutoka katika riwaya mbili (2) ulizosoma.

8. "Wasanii huwachora wahusika wao kuwa na tabia hasi na chanya." Jadili hoja hiyo kwa kutumia wahusika wanne (4) kutoka katika riwaya mbili (2) ulizosoma.

9. Jadili dhana ya mapenzi na ndoa kama ilivyojitokeza katika riwaya mbili (2) ulizosoma.

## SEHEMU D (alama 20)

### TAMTHILIYA

| | | |
|---|---|---|
| Kwenye Ukingo wa Thim | - | E. Hussein |
| Morani | - | E. Mbogo |
| Kivuli Kinaishi | - | Said Mohamed |
| Nguzo Mama | - | P. Mhando |

10. "Makosa yanatendwa na binadamu kwa kudhamiria au kwa uzembe." Fafanua hoja hiyo ukitumia mifano minne (4) kutoka katika tamthiliya mbili (2) kati ya hizo zilizoorodheshwa.

11. "Wanafasihi wengi huzungumzia uonevu kati ya kundi moja na jingine." Thibitisha usemi huo kwa kutumia hoja nne (4) kutoka katika tamthiliya mbili (2) ulizosoma.

12. Eleza namna vipengele mbalimbali vya fani vilivyotumiwa kujenga upevu wa tamthiliya mbili (2) ulizosoma. Fafanua maelezo yako kwa kutumia vipengele vinne (4) tofauti.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU E (alama 20)

## USANIFU WA MAANDISHI

13. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata:

Mimi ni kandambili, wengine huniita ndala. Vazi la chini sana katika mguu. Thamani yangu kwa watu, ni wakati wa kuoga. Wakimaliza hunitupa konani mwa nyumba na kuvaa viatu vya maana.

Uwaonao wamenivaa mchana kutwa ni wote wasio na uwezo. Wao hunitunza. Hunitunza kama mboni ya jicho. Ingawa naonekana sina thamani, umuhimu wangu ni mkubwa. Kuwasitiri wenye ukwasi na masikini.

Sijaona aendae kuoga, akaacha kunivaa. Sijaona aamkaye asubuhi, akaacha kunisalimu. Ninavyodharauliwa na kubezwa, inasikitisha! Wanivaao mchana wote huona aibu hawana viatu. Kandambili nina majina mengi. Wakati mwingine huniita malapa.

Navaliwa na kukanyagiwa majini. Viatu vya maana visioze. Kazi yangu kupambana na changarawe. Vipande vya chupa barabarani. Kazi yangu kupambana na miiba. Isiwachome wakulima shambani. Kazi yangu kupambana na wadudu, walioko msalani na bafuni. Mimi ndiye humsitiri mwenye kidonda. Asijitoneshe kwa kuvaa viatu vya maana. Viatu wenzangu mbona mnanicheka? Viatu wenzangu mbona mwanisengenya? Viatu wenzangu mbona mwanibinulia midomo? Asiyeweza kubuni hawezi kubaini. Wote tulijikuta tunaitwa viatu. Japo ninyi mmefunikwa.

**Maswali**

(a) Tashihisi ni nini? Eleza matumizi ya tashihisi kama yanavyojitokeza katika habari hiyo.

(b) Andika kichwa cha habari.

(c) Taswira ya kanda mbili yaweza kulinganishwa na nini?

(d) "Asiyeweza kubuni hawezi kubaini." Fafanua maana ya usemi huo ukizingatia ujumbe anaoutoa mwandishi katika habari hiyo.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

14. Soma habari ifuatayo, kisha eleza mbinu za kisanaa zilizotumika.

Mama: Juma hebu nitazamie hapo kama chungu changu kinachemka.

Juma: Haya.

Mama: Ebu nitazamie basi.

Juma: Ndiyo.

Mama: (Baada ya muda) Sasa wewe Juma husikii siyo? Umejipachika hapo viguu juu kama ndege; ukisemeshwa hujibu. Hata huyo korongo anatua chini kudondoa samaki.

Bibi: Hm!
Mwache ajisomee sasa. Kikichemka mimi nitakuambia. Mimi ninakiona kwa hapa.

Mama: Acha tumseme. Ukimfanyia hivyo ndivyo anazidi kichwa. Anajidekeza kama nini kwako huyo. Kaharibika siku hizi kama nini. Siku ile hapa nili----------.

Bibi: Chungu chako kinachemka. Mwanamke huachi mdomo. Ke, ke, ke, kama cherehani. Namna gani? Tabia mbaya.
(Mama anachukua nazi yake --- mbio anakwenda jikoni ----- ..Ajigonga)

Mama: Mama! Ayi! Ayi! Mungu wangu. Na hivi viti mnaweka mlangoni, hamuweki mahala pengine.

Juma: Sasa mimi niweke wapi? Nafasi yenyewe ndogo.

Bibi: (Kwa sauti ya kusengenya). Nyamaza. Jisomee hapo. Unamsikiliza mwendawazimu huyo.

Mama: (Anatoka jikoni). Nimesikia, nimesikia yote mliyokuwa mnasema. Lakini mimi kweli nitasema, Juma siku hizi amekuwa na roho mbaya. Siku ile mama yake Kitaru alikuja hapa kusema, "Kitaru mgonjwa. Anaumwa." Mimi nikauliza anaumwa? "Ndiyo anaumwa." Nikasema, "Akija Juma nitamwambia." Haya akaja Juma hapa mimi nikamwambia, "Juma rafiki yako anaumwa." Huyo mwenyewe mwulizeni kama ninamsingizia. Akajibu,. "Nimesikia." Basi nimesikia nimesikiaaa! Haramu kama mtoto alinyanyua unyayo --- unyayo bibi. Kaganda hapa juu ya kiti kama mfalme. Sema, uongo? Aaa, nisule.



TATA PRINT-2001

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Bibi: Sasa hakwenda wewe kinakuhusu nini?----. Afadhali aondoke. Ikisha kuwa huishi kumsumbua. Afadhali aondoke. Mtoto asirudi nyumbani. Akirudi tu, 'kwe, kwe, kwe, kwe, kwe, kwe'. Hm! Pole basi tena.

Mama: Kusema tutamsema – mtoto kiburi kimempita kimo.

Bibi: Afadhali amalize masomo yake apate kazi yake. Aepukane na adhabu hii. Na mimi nitamfuata huko huko uzunguni atakakokaa.



JATA PRINT 2013

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org